

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya simu "ADMIN"  
Simu ya mdomo 025 2552036  
FAX NO 0252552421 .



Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Rungwe,  
S.L.P 34,  
TUKUYU.

29/08/2023.

Unapojibu taja:-

Kumb. Na. AB.99/280/01/45

Maafisa Tarafa wote,

Watendaji wa Kata wote,

**WILAYA YA RUNGWE.**

**YAH: KUWATAARIFU WANANCHI KUHUSU TANGAZO LA UANDIKISHAJI WA  
VIJANA WA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA UTARATIBU WA  
KUJITOLEA (HIARI) MWAKA 2023/2024.**

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

2. Serikali ya Tanzania kupitia Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka wa fedha 2023/2024 litaandikisha Vijana wa kujitolea kwa hiari kutoka Vijijini na Mijini kwa Mkataba wa miaka miwili ya kulitumikia Taifa. Mnaombwa kuwaelekeza Vijana hao kuwa fursa hiyo ni kwa ajili ya kujifunza Uzalendo, Ukakamavu, Stadi za kazi na Stadi za maisha baada ya kumaliza muda wa Mafunzo na kurejea makwao na kuweza kujitegemea.


3. Kwa barua hii mnaelekezwa kuwataarifu wananchi katika maeneo yenu kuwa ratiba itaanza kama ifuatavyo: -

Tarehe 28/08/2023 – Tarehe 03/09/2023 – Kuwasilisha maombi.

Tarehe 04/09/2023 – Tarehe 05/09/2023 – Usaili ngazi ya Wilaya.

Sifa za waombaji zimeambatanishwa na barua hii.

Katika Ushirikiano.

  
Ally Said Kiumwa  
KATIBU TAWALA WILAYA  
RUNGWE

**Nakala:**

Mkuu wa Wilaya

**RUNGWE.** Aione ndani ya jalada.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

TAREHE 03/09/2023.



**Zifuatazo ni Sifa za Kuzingatia  
Katika zoezi la Kuwaandikisha Vijana**

1. Awe raia wa Tanzania.

2. **Umri.**

a. Kwa Vijana wenye Elimu ya Darasa la Saba umri ni kuanzia miaka **16** hadi **18**, waliomaliza Elimu ya Msingi kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Msingi

b. Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka **20**, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu wa Daraja la Kwanza hadi Daraja la Nne. Kijana mwenye Daraja la Nne awe na ufaulu wa alama kuanzia **26** hadi **32**.

c. Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka **22**, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu wa Kuanzia Daraja la Kwanza hadi Daraja la Nne.

d. Vijana wenye Elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka **25**, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

e. Vijana wenye Elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka **26**, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

f. Vijana wenye Elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka **30**, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

3. Awe na Afya njema, Akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).

4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
5. Awe na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho Kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
6. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).
7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo wala kuajiriwa na idara nyingine Serikalini.
8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa Kundi la Kujitolea na Kundi la lazima (Mujibu wa Sheria).
9. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
10. **Angalizo:** Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kali za kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

#### **Vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo JKT**

1. Bukta ya rangi 'Dark Blue' yenye mpira kiunoni (elastic) iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini isiyo na zipu, kwa vijana wa kike iwe na mpira kiunoni na kwenye pindo za miguu.
2. Raba za michezo zenye rangi ya kijani au blue.
3. Shuka mbili za kulalia zenye rangi ya blue bahari.
4. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
5. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenye baridi.
6. Truck suit ya rangi ya kijani au blue.
7. Flana ya kijani kibichi yenye kola ya duara isiyo na maandishi.
8. Nauli ya kwenda makambini na kurudi nyumbani.